JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

TAKUKURU KAGERA YAELIMISHA UMMA KUHUSU MADHARA YA RUSHWA KATIKA UCHAGUZI KWA NJIA YA BONANZA

TAARIFA KWA UMMA

Oktoba 26, 2020

1.0 Utangulizi

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera tumeendelea kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria namba 11 ya mwaka 2007. Katika utekelezaji wa majukumu yetu katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani tumeanza kushuhudia baadhi ya wanasiasa kuanza kutumia uwezo wao wa kifedha kuwashawishi baadhi ya wananchi kuwapigia kura kuliko hata kusikiliza sera za vyama vyao za kuwaletea maendeleo. Aidha katika kipindi hiki pia sio ajabu wananchi wapiga kura kuanza kuwashawishi wagombea kutoa rushwa ili wawapigie kura chini ya msemo maarufu wa wakazi wa huku usemao "wanisigota"

Ndugu wanahabari,

Kama mnavyofahamu, mwaka huu tarehe 28.10.2020 nchi yetu itafanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ambao watapewa dhamana ya kuwatumikia wa-tanzania kwa miaka mitano. TAKUKURU Mkoa wa Kagera tuliona ni vyema kuwakumbusha wananchi hasa wapiga kura, wagombea na viongozi wa vyama vya siasa juu ya umuhimu wa kuchagua viongozi waadilifu na wasiojihusisha na vitendo dhidi ya rushwa kwa maendeleo na maslahi mapana ya Taifa letu na kwamba ni wajibu wa kila mtanzania kuzingatia matakwa ya Sheria ya Uchaguzi na.1 ya mwaka 1985 inayojumuisha mapitio yaliyofanyika mwaka 2005 na Sheria zingine za nchi.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Kagera kutokana na hali hiyo ya uwepo wa viashiria vya rushwa na kuzingatia umuhimu wa uchaguzi tarehe 17.10.2020 katika Uwanja wa Kaitaba iliweza kufanya Bonanza la kuelimisha Umma kupitia michezo kwa kushirikiana na klabu kumi na moja vya wapinga rushwa mashuleni. Bonanza hilo liliandaliwa mahususi kwa lengo la kukemea vitendo dhidi ya rushwa wakati wa kampeni na wakati wa uchaguzi na lilisisitiza umuhimu wa kuchagua viongozi waadilifu.

Ndugu wanahabari,

Kauli mbiu ya Bonanza hilo ilikuwa **"KATAA RUSHWA, CHAGUA KIONGOZI MWADILIFU KWA MAENDELEO YA TAIFA**".

Kauli mbiu hii ilitokana na ukweli kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya Uadilifu na Rushwa. Uhusiano huu wa uadilifu na rushwa umeelezwa pia katika Maandiko matakatifu na yamehimiza na kusisitiza juu ya umuhimu wa uadilifu, kwa mfano Qur'an Takatifu katika Surat Nahil Sura 16, Aya ya 90 imeoyesha wazi ni kwa kiasi gani Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na kukataza uovu, uchafu na dhuluma. Aidha Kitabu cha Sunna za Abu Dawood hadithi namba 3573 imeelezwa wazi ni kwa kiasi gani Mwenyezi Mungu anamlaani mla rushwa yaani mtu apokeaye, atoaye na mshenga wa rushwa.

Ndugu wanahabari,

Pamoja na Qur'an takatifu kusisitiza uadilifu, Biblia takatifu pia imesisitiza uadilifu hususani katika kitabu cha Mithali 29:4 imesema wazi kuwa "Mfalme huthibitisha nchi kwa hukumu, bali yeye apokeaye rushwa huipindua" Katika kumbukumbu la torati 10:17 na Isaya 33:15-16 imefafanuliwa vizuri ni kwa jinsi gani Mwenyezi Mungu hataki dhuluma, upendeleo na rushwa. Hivyo kwa kuzingatia ukweli huu TAKUKURU Kagera tuliona tunalazimika kuielimisha jamii juu ya kuwachagua viongozi waadilifu, waaminifu na wazalendo wasiotokana na vitendo vya rushwa kwani hata maandiko matakatifu yanakemea uovu, dhuluma na rushwa na kuamrisha uadilifu na hivyo kumchagua mla rushwa ni kulifarakanisha taifa na muumba wake.

Ndugu wanahabari,

Katika bonanza hilo tuliweza kuelimisha jamii kwa kutumia michezo mbalimbali ikiwemo nyimbo, ngonjera, mashairi na mpira wa miguu.

Michezo hii iliweza kufafanua vyema dhana ya rushwa na athari ya rushwa katika uchaguzi. Aidha ujumbe uliotolewa katika uelimishaji huu ulikuwa na malengo makuu matano ambayo ni;

- Kuongeza uelewa kwa jamii juu ya madhara ya kumchagua kiongozi anayejihusisha na rushwa na/au asiye mwadilifu na kuhimiza uadilifu
- Kuongeza mshikamano, umoja na upendo miongoni mwa wananchi na kuipenda nchi yetu
- Kuwajengea vijana/wanachama wa Klabu za wapinga rushwa uwezo na ujasiri wa kukemea vitendo dhidi ya rushwa na kuichukia rushwa
- Kutoa burudani kwa jamii wakati wakipata elimu ili waweze kushirikiana na TAKUKURU
- Kufanya maonesho ya kazi zinazofanywa na TAKUKURU ikiwa ni pamoja na kugawa vipeperushi vyenye ujumbe wa mapambano dhidi ya rushwa lengo likiwa kuwa karibu zaidi na jamii

Malengo haya ya Bonanza yaliweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa na kwamba hii imeonekana kuwa ni njia bora ya kuelimisha jamii na mafaniko yalionekana kutokana na mwitikio mkubwa wa jamii na taarifa ambazo tumeendelea kupata kutoka kwa wadau baada ya Bonanza.

Ndugu wanahabari

Vitendo vya rushwa vimeendelea kuzitafuna nchi nyingi duniani kutokana na sababu mbalimbali, baadhi ya sababu zinazopelekea watu kujihusisha na vitendo dhidi ya rushwa ni mmomonyoko wa maadili miongoni mwa wanajamii, kukosekana kwa hofu ya Mungu, ubinafsi, tamaa ya mali, uchu wa madaraka, uelewa duni wa haki na wajibu wa

kila mwanajamii n.k. Ikumbukwe kuwa kukosekana kwa uadilifu ndiyo kisababishi cha sababu zingine na hivyo watu wameendelea kuwa wasaliti kwa jamii na kuendelea kujinufaisha kwa kutumia rasilimali za Taifa kwa manufaa binafsi.

Ndugu wanahabari,

Rushwa ikishamiri katika jamii huwa na madhara mengi. Baadhi ya madhara hayo ni pamoja na kuchaguliwa kwa viongozi wabovu wasiokuwa na sifa na uadilifu, humnyima mpiga kura haki ya kumchagua mgombea anayemtaka, inamnyima mgombea asiyetoa rushwa haki na fursa ya kuchaguliwa kuwa kiongozi wa kisiasa, hukwamisha utoaji wa haki ambapo haki hugeuka kuwa bidhaa inayouzwa na kununuliwa, husababisha kuongezeka kwa maovu katika jamii (uonevu, wizi, biashara haramu, mauji n.k), hudhorotesha maendeleo ya nchi, husababisha kuongezeka kwa migogoro, maradhi, ulemavu, vifo nk. Kutokana na watendaji kutowajibika ipasavyo kadri ya matakwa ya sheria na kufanya kazi kwa maslahi binafsi

Ndugu Wanahabari,

Bonanza la uelimishaji jamii lililofanyika lilianza na maandamano ambayo yaliongozwa na vijana wa Brass Band kutoka shule ya msingi ya Adolf Kolping ambao ni wanachama wa Klabu ya wapinga rushwa na pia lilihusisha wanachama na wanafunzi wa shule kumi za sekondari ambao ni wanachama na wasio wanachama wa Klabu za wapinga rushwa ambao wako mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya rushwa.

Aidha katika maandamano hayo viongozi wa Serikali, wananchi wapiga kura, waandishi wa habarui na baadhi ya wagombea walishiriki na hii

yote inaonyesha kuwa umma wa wana Kagera uko tayari katika mapambano dhidi ya rushwa.

Ndugu wanahabari,

Tunatoa wito kwa wananchi wote wa mkoa wa Kagera kuendelea kushirikiana na TAKUKURU na Serikali kwa ujumla katika mapambano dhidhi ya Rushwa kwani Rushwa ni usaliti kwa umma kwa sababu wala rushwa huweza kutumia rasilimali za taifa vibaya kwa maslahi binafsi kwa lengo la kujinufaisha wenyewe na hivyo hudhoofisha jitihada za za Serikali za kuleta maendeleo.

Ikumbukwe kuwa vitendo vya rushwa katika chaguzi za kisiasa vinaathiri mchakato mzima wa demokrasia ya uwakilishi na maendeleo ya taifa na hivyo tusikubali katu kumchagua mgombea mla rushwa au anayetumia ushawishi wa rushwa ili kuchaguliwa kama ambavyo vijana wanachama wa Klabu za wapinga rushwa wamebainisha katika nyimbo, mashairi na ngonjera wakati wa Bonanza.

Signed
JOHN K.E JOSEPH
MKUU WA TAKUKURU (M)